JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA AROBAINI NA TISA

**16 JUNI, 2017**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

### KIKAO CHA AROBAINI NA TISA – TAREHE 16 JUNI, 2017

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**399. MHESHIMIWA BONNAH MOSES KALUWA (SEGEREA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Katika Jimbo la Segerea zipo Shule kumi na moja za Sekondari za Serikali ambapo Wanafunzi wa Shule hizo wanafaulu vizuri kwa kupata daraja la I, II na la III na kuwa na sifa ya kujiunga na Kidato cha Tano kwa mfano mwaka 2015 Wanafunzi zaidi ya 400 walifaulu kwenda Kidato cha Tano; lakini katika Jimbo la Segerea hakuna hata Shule moja ya Kidato cha Tano licha ya kuwa na maeneo ya kujenga ya kutosha katika Shule za Sekondari za Kinyerezi, Magoza na Ilala:-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuanzisha Shule za Kidato cha Tano na Sita katika

maeneo ya Shule zilizotajwa ili kuwapunguzia Wanafunzi hao adha ya usafiri wanayopata kufuata Shule mbali.

**400. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Sheria ya Tawala za Mikoa Sura ya 97 inawapa mamlaka ya kipolisi Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwatia nguvuni watu kwa muda wa saa 48, lakini Sheria hiyo imekuwa ikitumiwa vibaya na Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa kutoa amri za kukamatwa kwa Wabunge, Wenyeviti wa Halmashauri, Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa, Vitongoji na hata Watumishi wa Umma wakiwemo Madaktari:-

(a) Je, Serikali inawachukulia hatua gani Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanaotumia vibaya madaraka na Sheria hiyo;

(b) Je, ni lini Serikali itaifanyia marekebisho Sheria hiyo ili kuwaondolea Wakuu wa Mikoa na Wilaya mamlaka ya kuweka watu ndani kwa kuwa ni kandamizi, inakiuka Haki za Binadamu na inatumika vibaya.

**401. MHESHIMIWA ISSA ALI MANGUNGU (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali ilitoa mafunzo kwa Walimu ambao walihitimu mwaka 2015 lakini Walimu hao hawajaweza kuajiriwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaajiri Walimu hao walioachwa ingawa kiuhalisia bado kuna uhaba mkubwa wa Walimu katika Shule za Sekondari hasa Vijijini.

## WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**402. MHESHIMIWA DANIEL NICODEMUS NSANZUGWANKO (KASULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Mahakama ya Wilaya ya Kasulu ni ya zamani sana, ni chakavu sana na wakati mwingine huduma hazitolewi kabisa:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali imeitelekeza Wilaya ya Kasulu;

(b) Je, Mahakama hiyo itajengwa lini.

## WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

### 403. MHESHIMIWA HAJI KHATIB KAI (MICHEWENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Serikali imeandaa utaratibu wa kuliwezesha Jeshi la Wananchi wa Tanzania kufanya shughuli zake kwa kulipatia posho mbalimbali ikiwemo *"ration allowance":-*

Je, ni lini Serikali itaiongeza posho hiyo ili iendane na maisha yalivyo sasa.

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

### 404. MHESHIMIWA OLIVER DANIEL SEMUGURUKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Katika maeneo ya Bugarama Wilayani Ngara kuna mgodi wa Kabanda Nickel uliodumu kwa miaka 30 sasa na Kampuni mbalimbali zimekuwa zikiendesha shughuli zake kwenye mgodi huo na kuondoka tangu Mwaka 1970 wakidai kuwa wanafanya utafiti huku bei ya Nickel katika soko la Dunia ikishuka:-

Je, ni lini Wananchi wa Ngara hususan wa maeneo ya Bugarama watanufaika na uwepo wa rasilimali hiyo iliyopo kwenye maeneo yao.

**405. MHESHIMIWA DKT. MARY MICHAEL NAGU (HANANG'):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Serikali imetoa kiasi cha Shilingi milioni mia tatu (300,000,000/=) kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji wa Katesh; hata hivyo mradi huo bado haujaweza kuwanufaisha Wananchi kwa sababu ya gharama kubwa za umeme zinazosababisha pampu za maji kufanya kazi kwa muda mfupi tu:-

Je, Serikali haioni haja ya kupunguza au kuondoa kabisa *tariff* zilizopo ili gharama ya umeme iwe chini kidogo na kusaidia kusambaza maji kwa ufanisi.

**WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

**406. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Wananchi wa Jimbo la Ndanda hawako tayari kabisa kuona mfumo wa uuzaji Korosho wa Stakabadhi Ghalani ukiendelea:-

Je, Serikali chini ya kauli mbiu ya 'Hapa Kazi Tu' ipo tayari kuondoa kabisa mfumo huo ambao ni kandamizi na hauendani na gharama za uzalishaji.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

### 407. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM MALEMBEKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne na Sita hufanyika kwa pamoja kwa Wanafunzi wa Tanzania Bara na Visiwani:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutumia Mitaala na Vitabu vya aina moja ili kuwapa Wanafunzi wa Zanzibar fursa ya kujisomea na kufanya vizuri katika Mitihani yao;

(b) Kwa kuwa Mitaala na Vitabu vya Elimu ya Awali na ya Msingi kwa upande wa Zanzibar ni tofauti na Tanzania Bara; Je, kwa nini Zanzibar wasiruhusiwe kutunga Mitihani ya Taifa tofauti na Bara kwa Kidato cha Nne na Sita na Mitihani hiyo ikapata hadhi sawa na ile inayotungwa Tanzania Bara.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA**
**16 JUNI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**